KUSOMA ACTIVITIES GRADE 3

Soma majina haya kwa sauti(Alama 6)

Sharubati	daktari
Foronya	daftari
Muhogo	shughuli
Majilisi	maktaba
Mbwa	makufuli

Soma hizi sentensi kwa sauti

Mama alinunua pipi thelathini

Lile ni gari jingine jeusi

Alhamisi hii tutaenda kumtembelea shangazi

Gwarideni pana karatasi nyingi sana

Mpira uko juu ya meza



Ni vizuri kuvuka barabara kwenye kivukio cha barabara

Mkoba maridadi umepotea

Mjomba alinipeleka kituoni cha basi

Nenda sokoni ukalete parachichi

Soma kifungu kifuatacho kwa sauti (Alama 6)

Mvua nyingi ikinyesha husababisha mafuriko. Wakati kuna mafuriko hutokea maafa na uharibifu mwingi wa mimea.Mchanga nao hubebwa na uzito wa maji yanayovuma kwa ukali kama simba. Watu hutoroka na kukimbilia mahali salama. Wengine huishia kupoteza mali yao yote na hivyo kuomba msaada kutoka kwa serikali na kwa wazalendo wenzao.